JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'

Simu Na. 027-2530022
Barua pepe:ded@hanangdc.go.tz
Tovuti:www.hanangdc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Hanang',
2 Barabara ya Amani,
S.L.P. 2,
27382 Ganana – Hanang',
MANYARA.

17/08/2023

TANGAZO LA KUKODISHA SHAMBA LA GAWAL NA BASSOTU.
ZABUNI NA. LGA/059/2023/2024/NC/04.

Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' inawatangazia wananchi wote, watu binafsi na Makampuni kuomba Zabuni ya ukodishaji wa mashamba ya Halmashauri yaliyopo eneo la Gawal lenye ukubwa wa ekari mia tano sabini na tatu (573) na Bassotu lenye ukubwa wa ekari elfu nane mia tano na sita nukta moja (8506.1). Mashamba yako kwenye maeneo mazuri yenye udongo wenye rutuba.

MASHARTI YA ZABUNI

1. Mwombaji wa Zabuni anatakiwa kulipa ada ya maombi ya Zabuni kiasi cha Tshs 50,000/= benki ya NMB baada ya kupewa control namba kutoka ofisi ya mweka hazina Halmashauri ambayo haitarudishwa.
2. Mwombaji wa Zabuni atapewa nyaraka za Zabuni "Tender Document" na Katibu wa Bodi ya Zabuni siku za kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa saa 2:00 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kuanzia tarehe 18/08/2023 hadi tarehe 06/09/2023. Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' katika ofisi ya manunuzi.
3. Nyaraka ya zabuni inatakiwa ijazwe kikamilifu na kusainiwa na Mtendaji wa Kijiji , Kata au Mtaa.
4. Mwombaji atakayeshinda Zabuni ataingia Mkataba wa msimu mmoja tu baada ya kulipia ekari alizoomba, kuanzia mwezi Septemba, 2023 hadi Agosti, 2024 na haruhusiwi kupanda mazao ambayo ukomavu/uvunaji wake utavuka msimu mwingine.
5. Mwombaji atakayeshinda Zabuni atatakiwa kulitumia shamba hilo kwa shughuli za kilimo tu na siyo shughuli nyingine kama vile ufugaji au uchungaji wa mifugo na ikiwa atafanya shughuli ambazo sio za kilimo Halmashauri itamnyang'anya shamba hilo bila kurejeshewa au kurudishiwa fedha za ukodishaji.
6. Ikiwa Mzabuni hatavuna mazao kutokana na hali ya hewa yaani ukame, mafuriko au wadudu waharibifu na mambo mengine ambayo yanafanana na haya, Halmashauri haitahusika na hasara hiyo.

7. Mzabuni atalazimika kutumia shamba kwa kuzalisha mazao ya chakula na biashara yanayokubalika kisheria (masharti ya zabuni yatahusika)
8. Halmashauri haitahusika na hasara itakayojitokeza katika kulima shamba atakalokodishiwa Mzabuni mfano:- ulinzi wa shamba, uharibifu unaotokana na mifugo na mengine yanayofanana na hayo maana yake ni kwamba majukumu yote yanayohusu shamba atakalokodishiwa ni juu ya mzabuni kuanzia Septemba 2023 hadi Agosti, 2024.
9. Mzabuni anatakiwa kutaja bei ya kukodisha shamba kwa ekari moja kwenye fomu iliyoambatanishwa.
10. Mzabuni hatakiwi kuharibu makinga maji "Contours" kwa ambayo yapo katika shamba kuyalima au kuyaondoa.
11. Mzabuni atatakiwa kulipa fedha zote za ukodishaji wa shamba ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kupewa barua ya kukubaliwa na ataingia mkataba na kupimiwa ekari alizolipia na kuoneshwa eneo lake ndani ya siku saba (7) baada ya kulipia.

12. Mwombaji wa Zabuni anaweza kupewa idadi ya ekari alizoomba au kupewa pungufu kwa kutegemea idadi ya waombaji.
13. Mzabuni atakayechukua zabuni ya shamba awe mhusika aliyepata shamba na siyo mwakilishi wake.
14. Utaratibu wa ugawaji wa shamba utakaotumika ni atakaye lipa wa kwanza ndiye ataanza kugawiwa shamba wakati wa ugawaji.
15. Hairuhusiwi mtu yeyote kulima shamba kabla ya kupewa au kugawiwa na Kamati ya ugawaji ili kuepuka mazoea ya kumiliki eneo na kuona kuwa mkodishaji anahaki ya kulima shamba hilo kila msimu bila kibali.
16. Kamati itagawa shamba kwa mhusika aliyekodisha shamba na siyo mwakilishi kulingana na maombi ya zabuni.
17. Mwombaji atakayejiongezea eneo bila Kamati kugawa shamba hilo halitakuwa kwenye umiliki wake na hatua za kisheria zitachukuliwa juu ya mkodishaji.
18. Mwombaji ataje eneo la shamba aidha Gawal au Bassotu kwenye barua yake ya maombi na ekari anazotaka na bei kwa kila ekari.

Barua zote za maombi ziandikwe kwa anuani ifuatayo:
KATIBU WA BODI YA ZABUNI
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'
S.L.P 2,
KATESH – HANANG'.

Juu ya bahasha iandikwe **ZABUNI YA UKODISHAJI SHAMBA LA HALMASHAURI LILILOKO GAWAL AU BASSOTU.**

19. Mwisho wa kuleta maombi na kupokea maombi ya Zabuni ni siku ya Juma tano tarehe 6/09/2023 saa 5:00 asubuhi kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang'.
20. Maombi ya zabuni ambayo yatawasilishwa baada ya muda wa mwisho wa zabuni iliyotajwa hayatapokelewa.

Francis E. Namaumbo
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HANANG'

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA
HANANG

NAKALA:

1. Ofisi ya Katibu Tawala. –Wilaya ya Hanang'
   S.L.P 10
   KATESH/HANANG'

2. Watendaji wa Kata wote - Wajulisheni wakulima katika Kata zenu.
   Halmashauri ya (W)
   KATESH/HANANG'

3. Mbao za Matangazo

MASHARTI YA ZABUNI YA UKODISHAJI WA SHAMBA LA BASSOTU/GAWAL MSIMU WA 2023/2024.

MWOMBAJI WA ZABUNI AANDIKE KUKUBALIANA NA MASHARTI HAPA CHINI:

NA	SHARTI	MZABUNI AANDIKE NENO: NAKUBALIANA AU SIKUBALIANI KATIKA CHUMBA KILICHOPO HAPO CHINI
1	Ada ya Zabuni Tshs 50,000.00.	
2	Mwombaji wa Zabuni ataingia Mkataba wa msimu mmoja kuanzia mwezi wa tisa (9) 2023 hadi mwezi wa nane (8) 2024.	
3	Mwombaji atakayeshinda Zabuni atatakiwa kulitumia shamba hilo kwa shughuli za kilimo tu na siyo shughuli zingine kama vile ufugaji au uchungaji wa mifugo	
4	Ikiwa Mzabuni hatavuna mazao kutokana na hali ya hewa yaani ukame, mafuriko au wadudu waharibifu na mambo mengine ambayo yanafanana na haya, Halmashauri haitahusika na hasara hiyo.	
5	Mzabuni anatakiwa kupanda mazao ambayo hayaleti uharibifu wa mazingira kulingana na Sheria inayotawala mazingira.	
6	Mzabuni anatakiwa kutoharibu makinga maji "Contours" ambayo yapo katika shamba kwa kuyalima au kuyaondoa.	
7	Halmashauri haitahusika na hasara itakayojitokeza katika kulima shamba atakalokodishiwa mfano: - ulinzi wa shamba, uharibifu unaotokana na mifugo na mengine yanayofanana na hayo maana yake ni kwamba majukumu yote yanayohusu shamba atakalokodishiwa mzabuni yatakuwa juu yake kuanzia mwezi wa tisa (9) 2023 hadi mwezi wa nane (8) 2024.	

8	Mzabuni atatakiwa kulipa fedha zote za ukodishaji wa shamba ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kupimiwa eneo lake, asipofanya hivyo atakuwa amekosa shamba.	
9	Kama kutatokea kutoeleweka au kutoelewana katika utekelezaji wa sharti lolote la Mkataba utakaofungwa kati ya Halmashauri na mshindi wa Zabuni (Mkulima) pande zote mbili zitakaa na kutatua tatizo kwa njia ya majadiliano. Ikiwa majadiliano yatashindwa kuleta muafaka suala hilo litapelekwa kwa msuluhishi ambaye ni Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tawi la Katesh na ikiwa usuluhishi utashindikana. shauri la suala hilo litapelekwa mahakamani	
10	Mwombaji wa Zabuni anaweza kupewa idadi ya ekari alizoomba au akapewa pungufu kutegemeana na idadi ya waombaji katika kundi aliloomba.	
11	**Taja idadi ya ekari.**	
12	**Taja kiasi utakacholipa kwa ekari moja.**	
13	**Taja eneo unalotaka kukodi aidha Gawal au Bassotu Plantation.**	

Mimi ..... nimesoma na kuelewa masharti namba moja mpaka namba kumi na tatu ya ukodishaji wa shamba la Bassotu/Gawal.

MZABUNI/MKULIMA;

JINA: .....

SAHIHI .....

SHAHIDI WA MZABUNI/MKULIMA;

(MTENDAJI WA KIJIJI AU KATA/MTAA)

JINA: .....

SAHIHI .....

MHURI WA OFISI